HOTUBA YA WN-OWM MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB) KATIKA SIKU YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI DUNIANI – IRINGA TAREHE 28 APRILI 2018

- Mheshimiwa Amina Masenza, Mkuu wa Mkoa wa Iringa;
- Bibi Hadija Mwenda, Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA;
- Viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA) na Chama cha Waajiri (ATE);
- Viongozi wa Serikali na Taasisi Binafsi mliopo hapa;
- Mabibi na Mabwana;
- Wageni Waalikwa

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia sote kuwepo hapa leo hii katika maadhimisho ya Siku

ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani, tukiwa wote wazima wa afya njema. Pia, napenda kuwashukuru nyote mliohudhuria katika maadhimisho haya kwani inaonesha kuwa nanyi mnaguswa na kuunga mkono jitihada zinazo chukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya afya na usalama sehemu za kazi.

Kadhalika, sina budi kuwashukuru waandaaji wa maadhimisho hayo ambayo yametukutanisha hapa leo na pia kwa kunipa nafasi ya kuwa mgeni rasmi na kuzungumza na ninyi katika siku hii muhimu tunapoungana na wenzetu duniani kote.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa mkoa wa Iringa hasa Mkuu wa Mkoa wa Iringa kwa kutukaribisha katika mkoa huu ili tuweze kuadhimisha siku hii. Hali kadhalika napenda kutoa

pongezi zangu za dhati kwa wadau wote ambao kwa namna moja ama nyingine wameshiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa siku hii ya leo inafanikiwa kama tunavyoona hivi sasa.

Mabibi na Mabwana,

Kama ilivyo kawaida yetu kila mwaka, tunapoadhimisha siku hii tunatumia kauli mbiu inayotumika duniani kote ambayo inatolewa na Shirika la Kazi la Duniani. Kauli mbiu ya mwaka huu ni **"Kizazi Salama chenye Afya – *Generation Safe and Health*".** Lakini katika mazingira ya nchi yetu kwa sasa ambapo tunajenga uchumi wa viwanda, kauli mbiu hiyo tumeitengeneza ili kuendana na mazingira ya sasa ya nchi yetu, ambapo kauli mbiu hiyo imeboreshwa na imekuwa ni ***"Kizazi Salama Chenye***

Afya kwa Uchumi wa Viwanda – Generation Safe and Health for Industrial Econmy"

Maana yake ni kuwa katika kujenga uchumi wa viwanda, pamoja na myororo wake wa thamani, ambao utafuatana na kuingiza teknolojia inayoambatana na vihatarishi vipya vya kiafya, ni vema sasa tukaongeza jitihada za kuwalinda wafanyakazi wetu hasa vijana. Pamoja na jitihada hizi itakuwa ni bora pia tukaendeleza mapambano ya kuondoa ajira mbaya za watoto.

Mabibi na Mabwana,

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, tunawaunga mkono wenzetu kote duniani kwa kuunganisha siku ya *Usalama na Afya mahali pa Kazi Duniani* pamoja na siku ya *Kukomesha Ajira mbaya za*

Watoto Duniani ambayo kwa kawaida inaadhimishwa tarehe 12 Juni ya kila Mwaka, ili kuimarisha kampeni ya kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi hasa vijana pamoja na kukomesha ajira mbaya za watoto. Kwetu sisi kama Nchi, msisitizo wetu ni juu ya ukuzaji wa uchumi wa viwanda sambamba na kuwalinda wafanyakazi vijana dhidi ya madhara yatokanayo na ukuaji wa viwanda pamoja na kukomesha ajira hatarishi za watoto.

Mwaka huu kampeni zinalenga kuharakisha utekelezaji wa vipengele vilivyomo kwenye Lengo namba nane (8) la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo ni kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wote ifikapo mwaka 2030 pamoja na kukomesha ajira mbaya za watoto ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia lengo hili kwa manufaa ya

kizazi kijacho tunahitaji makubaliano ya pamoja baina ya Utatu katika masuala ya kazi na ajira ikiwemo na kujenga utamaduni wa kujikinga na vihatarishi sehemu za kazi vinavyoweza kusababisha kuhatarisha afya na usalama wa wafanyakazi.

Mabibi na Mabwana,

Matokeo utafiti wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali uliofanyika mwaka 2014 na matokeo yake kuchapishwa mwaka 2016 yanaonesha kuwa watoto wenye umri kati miaka 5 – 17 walioko kwenye ajira ni takribani milioni 4.2 ambayo ni asilimia 28.8 ya wafanyakazi wote. Na katika hao asilimia 21.5 wako kwenye ajira hatarishi. Hali ni mbaya zaidi katika sehemu za mashambani ambako asilimia 35.6 ya wafanyakazi wote ni watoto. Watoto wengine wanajishughulisha na kazi katika sekta za madini,

misitu na uvuvi. Ripoti hiyo pia ilionyesha kuwa asilimia 11.1 (yaani 468,392) ya watoto waliopo kwenye ajira, walipata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi na wengine hata kupoteza maisha. Takwimu hizi zinaashiria kwamba, vijana wetu ambao tunawategemea kama nguvu kazi ya baadaye wanapata vilema vya maisha na wengine hata kupoteza maisha wakiwa katika hizo ajira za Watoto kila kunapokucha.

Mabibi na Mabwana,

Zipo changamoto nyingi zinawaweka vijana katika hali hatarishi wanapokuwa sehemu za kazi. Changamoto hizo ni kama vile hatua waliopo ya ukuaji wa kimwili na kisaikolojia, hali inayowafanya wao kuwa rahisi kudhurika na vihatarishi wakiwa kazini, ukosefu wa uzoefu kazini, ukosefu wa mafunzo

na stadi za kazi, kutokuwa na ufahamu wa kutosha juu vihatarishi katika sehemu zao za kazi pamoja na kukosa nguvu ya majadiliano kazini ambayo inapelekea kukubali kuajiriwa katika kazi hatarishi au katika kazi zenye mazingira mabaya ya kazi.

Hivyo, kampeni za mwaka huu zinalenga pia katika kutatua changamoto hizi na kuboresha mazingira ya kazi ya vijana na kufanya kazi iwe ya staha, kuzuia ajira hatarishi kwa vijana na watoto. Hii itakua ni sehemu ya mkakati madhubuti wa kuondoa kabisa aina zote za ajira kwa watoto na kuhakikisha kuwa watoto hao wanapata elimu bora kwa mujibu wa Sheria.

Na katika kuzuia ajira hatarishi kwa vijana wenye umri wa kufanya kazi, ni lazima waajiriwe katika kazi

zenye sifa ikiwemo kazi salama yenye hadhi, inayolinda heshima na utu wa kijana, yenye kuleta kipato stahili, inayoleta amani sehemu za kazi, inayotoa demokrasia, na yenye kukuza uchumi na kuongeza tija na pato la vijana na Nchi kwa ujumla. Na ili kazi iwe na sifa hizo ni lazima kudhibiti hali zote hatarishi zinazoweza kufanya mazingira ya kazi yasiwe salama.

Mabibi na Mabwana,

Mnamo mwaka 2006, Shirika la kazi Duniani (ILO) lilipitisha mkataba mpya wa kimataifa unaoitwa *"Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention (No. 187)".* Mkataba huo lengo lake ni kuweka msisitizo katika kutekeleza mikataba mingine iliyotangulia na itakayofuata ambayo yote kwa pamoja ni kuendelea kuboresha mazingira ya kazi

ili kuzuia ajali, magonjwa yatokanayo na kazi na vifo katika nchi wanachama wake. Katika kufanya hivyo msisitizo umewekwa katika mambo matatu makubwa ikiwemo suala la kuwa na Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi; pili kuweka mifumo imara ya utekelezaji wa sera hiyo kama vile sheria na mamlaka zinazopaswa kutekeleza sera hiyo; na tatu kuweka mikakati madhubuti ya utekelezaji. Wakati Serikali ya Tanzania inajiandaa kuridhia mkataba huo pamoja na mingine, tayari tumeishaanza utekelezaji wa baadhi ya mambo kama sehemu ya maandalizi. Mfano sera ya Taifa ya usalama na afya mahali pa kazi ipo tayari na kwa sasa inatumika. Marekebisho ya sheria ya usalama na afya mahali pa kazi nayo yameanza na kwa sasa yamefikia hatua nzuri. Mikakati ya utekelezaji sera itaanza kuandaliwa. Tuna imani kuwa mkataba huo na mingine mara itakaporidhiwa,

utekelezaji wake utakuwa rahisi na utasaidia kupunguza ajali katika sehemu za kazi kwa kuwa zitapungua kwa kiasi kikubwa.

Mabibi na Mabwana,

Ni vema kila tunapokutana kama hivi tukakumbushana suala la janga la UKIMWI kwa kuwa suala hilo ni sehemu ya usalama na afya mahali pa kazi. Janga hili linaathiri zaidi nguvu kazi inayotegemewa na Nchi hasa Vijana. Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa janga la ukimwi bado ni tatizo kwa nguvu kazi ya Nchi yetu. Kwa mujibu wa matokeo ya awali ya utafiti wa viashiria na matokeo ya ukimwi Tanzania wa mwaka 2016/17 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali – Zanzibar na kwa kushirikiana na wadau wengine yanaonyesha kuwa hali ya

maambukizi ya VVU imefikia asilimia 12 kwa wanawake wenye umri wa miaka 45-49 ikilinganishwa na asilimia 8.4 ya wanaume wenye umri wa miaka 40 – 44. Hali ya maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 – 24 ni asilimia 1.4 ambayo ni asilimia 2.1 kwa wanawake na asilimia 0.6 kwa wanaume.

Mabibi na Mabwana,

UKIMWI hauna tiba mpaka sasa pamoja na kuwa yapo madawa yanayofubaza makali ya virusi vya UKIMWI. Hivyo, tunapozungumzia mapambano dhidi ya UKIMWI, tuna maana mapambano ambayo ni zaidi ya matibabu.

Hatuna budi kutoa umuhimu wa pekee kwa wadau mbalimbali washirikiane katika mipango mizima ya kuzuia maambukizi mapya sehemu za kazi, kuondoa

unyanyapaa na ubaguzi, na kujaribu kuwasaidia wale wafanyakazi ambao tayari wameathirika kwa kuwapatia uwezo wa kula vizuri na ikiwezekana kuwawezesha kupata matibabu ya magonjwa nyemelezi kila yanopojitokeza. Kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeiokoa nguvu kazi ambayo inateketea kwa kasi kubwa. Napenda kuchukuwa nafasi hii kuwasihi wafanyakazi wote kwa hiyari yao wapime ili kuweza kujua afya zao na kuchukua hatua pale inapostahili. Lengo letu ni kufikia malengo ya 90-90-90 kwa watu wanaoishi na VVU ifikapo mwaka 2020; ambayo ni kifika asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU wawe wamejua hali yao ya maambukizi, asilimia 90 ya waliopimwa VVU na kugundulika kuwa wana maambukizi ya VVU wapatiwe dawa za kufubaza makali ya VVU na asilimia 90 ya watu

wanaotumia dawa za kufubaza VVU, iwe Virusi hivyo vimefubazwa kweli.

Mabibi na Mabwana,

Sekta isiyo rasmi na Wajasiriamali wenye Viwanda vidogo vidogo ni Sekta muhimu sana katika Maendeleo ya uchumi wa Nchi yetu. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika Mwaka 2014, inaonesha kuwa Sekta isiyorasmi inaajiri asilimia 21.7 ya wafanyakazi wote. Ukiachilia mbali changamoto za kutopata mitaji ya kufanyia shughuli zao hasa kutoka kwenye Taasisi za Kifedha, Wajasiriamali wanakabiliwa pia na suala zima la afya na usalama mahali pa kazi. Wajasiliamali hao wanakabiliwa na upungufu wa rasilimali fedha kugharimia huduma za afya na usalama kazini, ufahamu mdogo wa vihatarishi kazini, na ukosefu wa vifaa kinga, hali inayopelekea kutokea kwa ajali na

magojwa yatokanayo na kazi miongoni mwa wajasiriamali hao. Kwa maana hiyo, sisi kama Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine tunatoa elimu kwa wajasiriamali hao ili waweze kutambua na kuzuia vihatarishi vilivyopo katika mazingira yao. Mathalani katika kuelekea Maadhimisho ya siku ya leo na kama sehemu ya kampeni hizi, nimetaarifiwa kuwa wajasiriamali 4,500 katika sekta ya madini kutoka Mikoa ya Shinyinga, Geita, Manyara (Merelani), Lindi, Mbeya, Dar-es-Salaam, na Dodoma wamepatiwa Elimu.

Serikali pia inathamini juhudi za makampuni ya umma na binafsi au waajiri kwa ujumla kwa kushirikiana na wafanyakazi wanaojituma katika kuboresha mazingira ya kazi kwa mujibu wa sheria na waajiri wote wanaofanya ubunifu wa kuboresha mazingira ya

kazi wao wenyewe bila kushurutishwa. Hivyo kwa kupitia Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA), Serikali imeanzisha Tuzo Maalum kwa watu watakaokuwa wanaonesha juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi kwa kuweka mifumo ya afya na usalama kazini iliyo imara na inayoleta tija katika sehemu za kazi. Mwaka huu ni mara nyingine tena kutoa tuzo hii. Tutaendelea kuboresha shindano hili kila mwaka hadi itakapofikia kiwango cha kuridhisha. Napenda kuchukua furusa hii kuzipongeza kampuni zilizofanikiwa kupata tuzo kwa mwaka huu.

Mabibi na Mabwana,

Mwisho, ningependa kusisitiza kuwa, Serikali ya awamu ya tano kamwe haitapuuza suala la usalama na afya mahala pa kazi hasa wakati huu tunapojenga uchumi wa viwanda ambao utaambatana na

vihatarishi vingi vipya. Kwa hivyo, itaendelea kushirikiana na wadau wote ili kupunguza au hata ikiwezekana kuondoa kabisa vifo, ajali, magonjwa na madhara yatokanayo na kazi.

Baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru wote mlioshiriki kikamilifu katika maadhimisho haya na ninawatakia mchana mwema.

Ahsante kwa kunisikiliza